



Schweizerische Eidgenossenschaft
Confédération suisse
Confederazione Svizzera
Confederaziun svizra

Embassy of Switzerland in Tanzania
Ubalozi wa Uswisi Tanzania



50 Years of Diplomatic Relations.

Tanzania.
Switzerland.

USWISI NA TANZANIA WASHEHEREKEA MIAKA 50 YA USHIRIKIANO WA KIDIPLOMASIA

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Dar es Salaam, Oktoba 20 2016 – Mwaka huu ni wa maadhisho ya miaka 50 ya ushirikiano wa kidiplomasia kati ya Uswisi na Tanzania. Ili kusheherekeea tukio hili, Ubalozi wa Uswisi leo umezindua kitabu ‘A Concise Study of Contemporary Art in Tanzania’, kama ishara ya urafiki wa muda mrefu kati ya nchi hizi mbili na watu wake. Kitabu hicho kilizinduliwa rasmi na Makamu wa Rais wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan Ikulu leo.

Kitabu pia kitaonyeshwa katika sherehe ya kuadhimisha miaka 50 ya ushirikiano baina ya nchi hizo Ijumaa Oktoba 20 Nyumbani kwa Balozi ambapo itaambatana na maonyesho ya kazi za wasanii amabazo pia zipo ndani ya kitabu hicho. Maonyesho hayo yataendelea siku inayofuata, Jumamosi Oktoba 22, na pia kutakuwa na majadiliano (roundtable discussion) kuhusu sanaa ya uchoraji wa kisasa nchini Tanzania. Majadiliano hayo yatakuwa na wazungumzaji mahiri akiwepo Prof. Elias E. Jengo, profesa wa Sanaa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Yves Goscinnny, mwandishi wa kitabu ‘A Concise Study of Contemporary Art in Tanzania’.

Katika kipindi cha miaka 50 iliyopita, Uswisi na Tanzania zimejenga ushirikiano mzuri kuitia majadiliano ya kisiasa, ushirikiano wa kiuchumi na maendeleo, na katika shughuli za utamaduni. Katika hotuba yake, Balozi wa Uswisi nchini Tanzania, Mheshimiwa Florence Tinguely Mattli alisema kipindi cha miaka hamsini nchi hizo mbili zimeshuhudia ushirikiano kati yao ukiendelea kuimarika kutokana na heshima na maelewano, na dhamira kubwa ya maendeleo ya binadamu. “Kuitia juhudi za pamoja, ushirikiano kati ya Tanzania na Uswisi uameleta mafanikio mengi katika mahusiano ya kisiasa na maendeleo. Ushirikiano huu umekuwa na manufaa kwa nchi zote mbili, hasa katika sekta ya afya. Mafanikio haya yanatupa sababu ya kutafakari historia ya muda mrefu ya mahusiano mazuri na kusheherekeea miaka 50 ya urafiki kama msingi imara wa ushirikiano. Na ubunifu wa sanaa ya Tanzania uhamasishe ushirikiano wetu kwa miaka 50 ijayo!” alisema.

Mkataba wa Ushirikiano kati ya Uswisi na Tanzania

Uhusiano wa kibalozi kati ya Uswisi na Tanzania uliimarika baada ya ufunguzi wa Ubalozi mwaka 1996 na kutiwa saini ya makubaliano ya ushirikiano wa kiufundi na kisayansi. Kabla ya hapo, wamishenari, wakulima na wafanyabiashara wa kiswisi wamekuwa wakifanya shughuli zao nchini Tanzania tangu miaka ya 1920. Mwaka 1927 Uswisi ilifungua Ubalozi Mdogo mjini Tanga ambapo Uswisi ilikuwa imewekeza katika sekta ya mkonge. Baadaye Ubalozi Mdogo ulikuja kuhamishiwa Dar es Salaam mwaka 1961. Uswisi na Tanzania imesaini mfululizo wa mikataba ya kuimariha mahusiano baina ya nchi hizo mbili, hasa juu ya ushirikiano wa kiufundi na kisayansi (1966), usafiri wa anga (2004), na ulinzi na uwekezaji (2004).

Shirika la Maendeleo na Ushirikiano la Uswisi (SDC)

Tangu miaka ya 1950, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, watafiti na wataalamu wa Kiswisi wamekuwa wakitoa msaada wa kifundi na kifedha nchini Tanzania. Uswisi imekuwa ikisaidia miradi ya maendeleo nchini Tanzania tangu miaka ya 1960. Shughuli zake ziliongezeka mwaka 1981 ilipofunguliwa ofisi ya ushirikiano wa maendeleo jijini Dar es Salaam. Uswisi inaendelea kufanya kazi na washirika wa Tanzania na Uswisi ili kusaidia kuleta usawa wa kijamii, ukuaji wa uchumi ambao ni shirikishi kwa raia wote, na kupunguza umaskini katika mikoa maskini ya Tanzania kuitia sekta tatu muhimu za afya, ajira na kipato, na utawala.